HALI YA MIUNDO MBINU YA BARABARA

Mkoa ulipoanzishwa Mwaka 2012, ulikuwa na jumla ya km. 6,403.45 za barabara ambazo zilikuwa zimegawanyika katika Halmashauri na “TANROADS” kama ifuatavyo:

- Mji wa Njombe Km.1,315.3, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Km. 848.8, Halmashauri ya Wilaya Ludewa Km. 963.43, Halmashauri ya Wilaya Makete Km. 767.8, Halmashauri ya Wilaya ya Wanging’ombe Km. 896.9, Halmashauri ya Mji Makambako km 484.8 na TANROADS ina jumla ya Kilomita 1,123.42.
- Barabara zilizokuwa zinahudumiwa na mfuko wa barabara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ni jumla ya kilometa 970 kwa halmashauri 558 kilometa na 412 kilometa ikiwa kwa mwaka 2015 jumla ya kilometa 2230.52 ambazo ni asilimia 15-35.

- Barabara za Lami zilikuwa hazipo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo kwa kipindi hiki jumla ya Km. 33.55 zinaendelea kujengwa na zilizokamilika kwa mgawanyo ufuatao:-

Ludewa Km.6.75; Halmashauri ya Mji Njombe Km.4.2; Makete Km.14 na Kilomita 5.6 zimeanza kujengwa katika Wilaya mpya ya Wanging’ombe na jumla ya km. 3 Mji wa Makambako.

Aidha, Wakala wa barabara Mkoa (TANROADS) wameendelea kujenga barabara kwa kiwango cha lami na changarawe, kufanyia matengenezo ya kawaida barabara zilizopo, kujenga madaraja na makalvati ili barabara ziweze kupitika kwa wakati wote katika maeneo yote ya Mkoa. Utekelezaji uliofanyika kuanzia mwaka 2005 hadi sasa ni kama ifuatavyo:

- Ujenzi wa barabara ya Njombe - Makete kwa kiwango cha lami (km 12.5). Barabara hiyo ilikamilika kwa gharama ya shilingi 5,363,922,000/=.

- Ujenzi wa barabara ya Njombe - Makete (km. 4.3) Njombe Mjini na Chalowe, Igwachanya (km1) kwa kiwango cha lami. Gharama iliyotumika ni kiasi cha shilingi 2,259,762,900/=
- Ujenzi wa barabara ya Igwachanya Mjini kwa kiwango cha lami (km. 2). Barabara ilikamilika kwa gharama ya shilingi 1,299,394,500/=
- Ujenzi wa barabara ya Njombe – Ramadhani – Iyayi kwa kiwango cha lami (km. 2). Gharama zilizotumika ni kiasi cha shilingi 1,154,625,605/=
- Ujenzi wa barabara ya Njombe – Makete (km. 1.5) na Njombe Mjini (km.0.2). Barabara ikikamilika itagharimu kiasi cha shilingi 1,028,975,900/=.
- Ujenzi wa barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 6.75). Gharama iliyotumika ni shilingi 1,028,975,900/=.
- Kupanua barabara (Spot Improvement) Ludewa – Lupingu (km. 28). Fedha iliyotumika ni shilingi 691,500,000/=.
- Ukarabati wa barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (sehemu ya Itoni – Mkiu). Barabara ilikamilika kwa gharama ya shilingi 2,552,495,000/=.
- Ukarabati wa barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (sehemu ya Mkiu – Ludewa) (km. 70). Gharama zilizotumika ni shilingi 2,552,425,000/=.
- Ukarabati wa sehemu ya barabara ya Ludewa – Nkomang'ombe na barabara ya Mchuchuma kuingia Mchuchuma. Ujenzi umekamilika na gharama zilizotumika ni shilingi 1,596,277,000/=
- Ukarabati wa sehemu ya barabara ya Mkiu – Mundindi (Liganga) (km 46). Ujenzi umekamilika na gharama zilizotumika ni shilingi 1,709,706,500/=.
- Ukarabati wa barabara ya TANZAM Highway na ujenzi wa barabara ya Ramadhani (Njombe) – Iyayi kwa kiwango cha lami (km 4.5). Ujenzi unaendelea na gharama zilizokadiriwa kutumika ni shilingi 1,863,000,000/=.

Pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo, pia kuna miradi ya barabara mikubwa ambayo ipo katika hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

- Njombe – Ndulamo Makete km 109.4 Mhandisi mshauri M/s Crown Tech yupo katika hatua za mwisho za kumalizia kazi hiyo.

- Kibena – Lupembe – Madeke km 126.18 Mhandisi Mshauri M/s Howard Humphreys Consulting Co yupo katika hatua za mwisho za kumalizia kazi hiyo.
- Itoni – Luldewa – Manda km 211.4 Mhandisi Mshauri M/s Crown Tech Consult anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifuwa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.
- Njombe (Ramadhani) – Iyayi km 73.97 na Chalowe – Igwachanya km 7.34. Mhandisi Mshauri M/s Afrisa Consulting Co anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.
- Ukarabati wa barabara ya Mafinga – Igawa (km 142) taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri (Technical Consultant) kwa ajili ya usimamizi wa ukarabati wa barabara zinaendelea na zipo kwenye hatua za mwisho.Taratibu za tathmini za zabuni za kumpata Mkandarasi wa ukarabati zinaendelea na zabuni zimefunguliwa tarehe 26 Mei, 2014. Ukarabati utafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Dunia (IDA).

- Ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea (KM. 295) taarifa za usanifu wa kina tayari zimewasilishwa na kupitiwa kwa ajili ya utekelezaji.

- Hali ya kupitika kwa barabara za vijijini imeboreshwa na kufikia hatua ya kupitika kwa asilimia zifuatazo:-

(i) Njombe Mji toka asilimia 50 hadi 85%
(ii) Halmashauri ya Wilaya Njombe toka asilimia 55 hadi 80%
(iii) Halmashauri ya Wilaya Ludewa toka asilimia 55 hadi 85%
(iv) Halmashauri ya Wilaya Makete toka asilimia 45 hadi 80%
(v) Halmashauri ya Mji Makambako toka asilimia 65 hadi 90%
(vi) Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe toka asilimia 65 hadi 90%
(vii) Wakala wa barabara TANROADS toka asilimia 60 hadi 95%

Hali hii imepelekea wastani wa upitikaji wa Barabara zote za Changarawe, Udongo na Lami kuwa asilimia 77 Ki-Mkoa.

Serikali imeendelea kuimarisha Mfuko wa Barabara “Road fund” na fedha za maendeleo ili kuongeza kasi ya Ukarabati na ujenzi wa Miundombinu. Fedha za kuhudumia Barabara zimeendelea kuongezeka ambapo Mwaka wa fedha 2013/2014 Jumla ya Shilingi 16.7 Bilioni zilipangwa kutumika Mkoani ambapo Halmashauri zilitengewa Shilingi 5.0 Bilioni na Wakala wa Barabara (TANROADS) Shilingi 11.7 Bilioni. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 jumla ya shilingi 27.027 bilioni zitatumika ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 11 ukilinganisha na mwaka 2013/2014.

Taarifa ya Urefu wa Barabara za Mkoa wa Njombe mwaka 2005 na 2014

s/na./mwaka	**2005/06 (urefu wa barabara)**			**2014/15 (urefu wa barabara)**			**ongezeko kwa asilimia**	
	Lami	**changarawe**	**udongo**	**lami**	**changarawe**	**udongo**	**lami**	**changarawe**
HALMASHAURI	5.9	484.41	5913.45	33.55	2600	3769.9	0.1-0.5	8-41
WAKALA WA BARABARA	192.56	315	615.86	210.16	913.26	0.0	18-19	28-81

Taarifa za Fedha kwa ajili ya Barabara Mkoa wa Njombe kutoka Mfuko wa barabara na Mfuko wa Maendeleo (2005-2014)

s/no	**Mwaka**	**2005/06**	**2014/15**	**Ongezeko kwa asilimia**
1	HALMASHAURI	1,000,000,000.00	10,417,548,120.00	8.6-91.2
2	WAKALA WA BARABARA	4,300,000,000.00	17,027,256,000.00	20.2-79.83